**SEHEMU YA KWANZA**
**HISTORIA, FALSAFA NA MAKUSUDI YA CHAMA CHA WAVUMBUZI**

**KUSUDI:**
Kuhimiza kuwa utume na makusudi ya kanisa la Waadventista wasabato yanapaswa kuwa yenye msingi na manufaa kwa familia zetu za kizazi hiki.

**LENGO:**
Kutambua kuwa falsafa, makusudi na umakini wa huduma za wavumbuzi na kupata historia nzima ya wavumbuzi.

**MAELEZO**

1. **Historia**

   Program za wavumbuzi ziliznzishwa ili kusaidia wazazi katika jukumu muhimu la malezi yao wakiwa kama walimu wa kwanza na mwinjilisti. Zimekusudiwa kukomaza mahusiano ya wazazi na watoto kiroho, kimwili, kiakili na kijamii.
   Mwaka 1939 G.C. ilianzisha wazo la madarasa ya wavumbuzi, Nyuki wa shughuli, Mwali wa jua, Mjenzi na Mkono wa Msaada.
   Mwaka 1972 kanisa lilidhamini kongamano la wavumbuzi kule Washington lililoitwa “Beavers”
   Mwaka 1980 – Conference nyingi zilikuwa zimedhamini watoto wao (Wavumbuzi)
   Mwaka1980 – Amerika ya kasikazini iliita wataalamu wa watoto na kuunda kamati ya kutathimini program za wavumbuzi.
   Mwaka 1989 – Kuanzishwa nishani za wavumbuzi na program zake zikaboreshwa.

2. **NEMBO YA WAVUMBUZI**

   Ni sehemu ya utambulisho inaonyesha namna watoto hawa wanavyoshughulika na kanuni inayoendelea kujitokeza katika maisha yao na kuanza kazi ya injili ya Bwana wetu Yesu Kristo

3. **FALSAFA**

   Chama cha wavumbuzi huduma iliyodhaminiwa na kanisa la waadventista wasabato, ambapo wazazi, kanisa, shule zinashirikiana pamoja na kuunga mkono kumsaidia motto kukua kwa furaha katika hekima na kimo wakimpendeza Mungu na wanadamu. Pia kusaidia wazazi kufanya watoto kukua kwao kuwe na maana. Tukitambua kuwa watoto ndiyo mtaji mkuu wa kanisa (Mwongozo uk. 2)

4. **WAVUMBUZI KAMA HUDUMA**

   a) **Malengo na makusudi**

      Program hizi zimekusudiwa kumuunga mkono mzazi katika wajibu wao muhimu kama walimu na wainjilisti wa kwanza wa watoto hawa.

      **Hivyo huduma inalenga**

      i. Kufanya mtoto kutoa maisha yake kwa Yesu katika umri wake.
      ii. Kumpa mototo tabia chanya ya kupata faida ya upendeo na majukumu ya kupenda maisha ya ukristo.
      iii. Watoto wapate tabia, ujuzi na ufahamu unaohitajika kwa kuishi na Yesu.
      iv. Wazazi na walezi wawe na uthibitifu wa mafanikio kama watendao kazi pamoja na Yesu.

**MAKUSUDI**

i. Kukuza tabia ya Yesu ndani yao
ii. Kufurahia kufanya vitu vizuri
iii. Kuonyesha tabia ya Yesu katika uhalisi wao
iv. Kugundua vipawa vyao na kuvitunza.
v. Kukuza uwezo wao wa kucheza na kuhusiana na wengine.
vi. Kuvumbua thamani ya Neno la Mungu.
vii. Kuwasaidia kugundua nini kinachofanya familia zinakuwa zenye furaha.

**b) Kanisa**

Ndiye mdhamini mkuu wa klab hii, hivyo viongozi wanapaswa wawe karibu na chama hiki.

**c) Jamii**

Tunapoongea jamii tuna maana ya idara za familia, shule sabato, idara ya watoto, washiriki, wanapaswa kuwa vyanzo vizuri vya kukomaza idara hii leo idara hizi zinaonekana kuwa wavumbuzi siyo sehemu ya majukumu yao.

5. **KANUNI YA KUFUNDISHA YA WAVUMB**UZI

Kanuni au mwongozo umejaa kila kitu cha muhimu ambamcho mwalimu, mzazi, mlezi anachopaswa kufahamu kuwaongoza watoto hawa kwa mafanikio, ziko shughuli nyingi zinazopatikana katika miongozo soma zielewe, usifundishe kutumia uzoefu, utakosesha.
Mwongozo unaelekeza program zote zinazotakiwa kwa kila hitaji, unahimizwa kutumia.

## SEHEMU YA PILI
## KUWAELEWA WAVUMBUZI Kipindi dk 60

**KUSUDI:**

Kwa nini tunajifunza kuwaelewa wavumbuzi ili kuwahudumia vyema kulingana na mahitaji yao.
Kuwasaidia wazazi, walimu, walezo kutokana na changamoto za kuongoza watoto katika kumpokea Yesu.

**MALENGO:**

Kutambua maendeleo ya ukuaji wa mahitaji ya wavumbuzi na kujifunza namna ya kushughulikia mahitaji yao kwa mafanikio.

**MAELEZO:**

Anaeshiriki kazoo hii aelewe na kujadili yafuatayo.

1. Maendeleo ya ukuaji wa tabia za watoto wa miaka 6 – 9
   - Tunahitaji kutambua kuwa toka mimba inapotungwa ndani ya tumbo la mama, darasa/mafunzo kwa mototo yanaanza. Anapozaliwa unapaswa kuendelea kuzikuza tabia uzitakazo kwa mtoto .

- Ndiyo sababu kabla hajashughulika na mtoto unapaswa kufahamu watoto siku zote kuanzia siku anapozaliwa, anataka kujua anachosikia anachoona na wanachokutana nacho katika uzoefu wa maisha yake, kwa misingi hiyo tunahitaji usikivu wetu tuuweke katika mahitaji mbalimbali yanayojitokeza kwa watoto hawa, na pia ni kwa jinsi gani tunawatendea.
- Tabia zao zinategemea zaidi wale wanaohusiana nao kila siku katika maisha yao.
- Kadri wanavyokuwa viungo vyao vyafahamu vinafunguka zaidi kupokea na kukabiliana na kile kinachogusa maisha yao.

**Tabia ya kimwili**:

i. Wananguvu nyingi
ii. Mwili wao unaratibu mambo mema

**Kiakili:**

i. Wajifunze zaidi kwa kutenda
ii. Wana hamu ya kujua kila kitu
iii. Anaelewa zaidi kile anachoona na kugusa.
iv. Ni watu wa kupiga taswira katika bongo zao
v. Wanakariri vyema
vi. Wanapenda vitu vya namna mbalimbali

**Misukumo ya jamii**:

i. Wanajifunza stadi za jamii.
ii. Wanapenda kujitegemea, kufanya mambo wenyewe.
iii. Wanahitaji mafanikio na kuthibitishwa na mzazi, mlezi, mwalimu/washiriki.
iv. Wanahamasika kirahisi.
v. Wanapenda jamii.

**Kiroho**

i. Wako makini kufuatisha kitu kibaya na kizuri.
ii. Bado wanahamasishwa na faida ya binafsi.
iii. Elimu ya maandiko wanaifyonza sana.

**Wanaitikiaje:** kwa tabia hizo unapaswa kufanya yafuatayo:

i. Wasikae mahali pamoja kwa muda mrefu.
ii. Wanapenda michezo kwa wingi ili kuratibu viungo vyao.
iii. Usiwe wa kueleza tu mambo wape wafanye kwa mikono yao.
iv. Wanataka kufahamu ulimwengu unaowazunguka panga ziara, waeleze vitu vya kuvutia.
v. Usiwe na maelezo marefu, mwambie mara moja apaswacho kufanya, maelezo marefu hawashiki.
vi. Wanapenda visa na hadithi
vii. Wanapenda nyimbo, michezo na shughuli
viii. Wape nafasi za kuhusiana na wenzao
ix. Mfanye atafute njia za kufanya vitu vizuri.
x. Wanapenda kucheza na kuongea na marafiki.
xi. Wasaidie kutambua kilicho haki na kwa nini sheria ni muhimu.
xii. Wanahitaji msingi imara wa kibiblia

xiii. Wako tayari kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wao.

Utakapofanya au kufuata maelekezo haya wataitikia sana kile unachotaka wafanye

**2. Matokeo ya makundi ya rika lao**

- Wanapenda kucheza na kuongea na rafiki zao
- Ni wepesi wa kuiga kile mwenzake anachofanya
- Hivyo tabia ya rika lao inawaathiri haraka kwa mabaya au kwa mema ikitegemea na kundi alilonalo.

**3. Kanuni za mafanikio za nidhamu ya chama**

**a) Nidhamu dhidi ya adhabu**

Watoto hawa wafundishwe wazi kuwa Mungu anapendezwa na utii. Wajenge mawazo kuwa Mungu anapendezwa na maisha yao yote, wasaidie kujifunza zaidi upendo wa Mungu, wape kutofautisha kati ya nidhamu na adhabu. Tunataka wawe wanafunzi wa Yesu jambo hili kimsingi ni kiusahihi nidhamu siyo adhabu bali ni kuongoza vijana kutawala mambo yao.

**b) Usalama wa klab yako**

i. Watoto wote kwa shughuli zao walipiwe bima.
ii. Hakikisha mahali wanapofanya shughuli zao kuna usalama.
iii. Usiwape kazi zinazotishia usalama wao.

**c) Unyanyasaji wa watoto**

Elewa aina za unyanyasaji – uchunguzi unaonyesha zipo aina 8 za unayanyasaji

i. Kupuuza mtoto katika mahitaji ya kimwili
ii. Kupuuza kuwapa maadili mema
iii. Kutowahudumia wanapoumwa
iv. Kutowapa elimu bora wanayopaswa kuipata.
v. Kuwapiga kusikositahili
vi. Kuwahitaji kufanya nao ngono
vii. Jamii au kanisa kutowajali kwa mahitaji yao
viii. Kupuuza hisia zao

Tunapowahudumia hayo tunapaswa kuyaangali sana

**d) Kuwanyanyasa kingono**

Huku kunarahisihsa hasa kuwabaka na kuteswa kwa nguvu kingono. Hii sasa katika jamii limezagaa kati ya wasichana wane katika jamii mmoja amebakwa au kunyanyaswa kingono kabla ya miaka 18 na wengine wamelawitiwa.

**4. Wavumbuzi kama watu muhimu**

Hawa vijana ni muhimu sana maana ndiyo miaka yao ya kujenga tabia yao ya maisha ya sasa nay a umilele. Tunapaswa kuwashughulikia kwa hali zote ili kuwaandaa kwa maisha bora ya leo na ya umilele.

## SEHEMU YA TATU

## UONGOZI – Kipindi dak. 60

**Kusudi**
Kujifunza dhana na mikakati ya upate uzoefu wa kufanikiwa katika uongozi wa wavumbuzi.

**Lengo**
Kuelewa aina mbali mbali za mtindo wa uongozi na namna unavyoleta matokeo katika umri mbalimbali

**MAELEZO**
Washiriki wajadili matazamio ya uongozi wa kikristo kwa klabu ya wavumbuzi

1. Ni nini maana ya uongozi …………………………………………………………
2. Mtindo wa uongozi – zipo aina nne
   a. Auto crafic …………………………………………………………...

   b. Kuruhusu kila mtu afanye atakavyo
   ……………………………………………………………………………..

   c. Democratic …………………………………………………………...

   d. Authorization …………………………………………………………...

3. Mwenendo na sifa za uongozi wa kikristo
   i. ……………………………………………………………………………..
   ii. ……………………………………………………………………………..
   iii. ……………………………………………………………………………..
   iv. ……………………………………………………………………………..
   v. ……………………………………………………………………………..

**4. KAZI ZA VIONGOZI**

**Mkurugenzi**
- Ni kiongozi wa mambo yote ya chama.
- Mwenyekiti wa Baraza
- Mjumbe wa baraza la kanisa
- Kiungo kazi yake na mchungaji na viongozi wa kanisa
- Msimamizi wa kazi zote
- Kusaidiana katika kupanga mipango yote

**Msaidizi**
- Msimamizi wa masomo ya madarasa
- Msimamizi wa maburudisho
- Kusumamia mziki.

**Karani**

- Kukagua makadi ya Wavumbuzi
- Kukusanya point zote
- Kujaza taarifa ya kila robo
- Kutayarisha matangazo
- Kupokea taarifa
- Mwandishi wa miniti za baraza la wavumbuzi.

**Mshauri**
- Ni mmoja wa wajumbe wa baraza la wavumbuzi
- Ni mwangalizi wa vikosi vya vijana vya watu 4 – 8
- Anapaswa kuhudhuria kila mkutano
- Wafahamu wanachama wote
- Anayepaswa kuona kuwa kanuni zote za watoto zinafuatwa
- Atowe mfano wa usafi, uchangamfu avae sare
- Kutiwa moyo vijana kuhudhuria shughuli za wavumbuzi
- Kuhudhuria mikutano yote.

**5. MASWALI YA NAMNA YA KUWEKA MAGOLI YA VITU VYA KUTAFAKARI**

Unapokuwa kiongozi maswali yafuatayo ndiyo ya kujiuliza

a) Unataka kukamilisha nini?
b) Utayakamilishaje?
c) Utayakamilisha wakati gani?
d) Nani atawajibika?
e) Vitu vya kutawala
f) Hatua za mawasiliano.

## SEHEMU YA NNE

**MUUNDO WA CHAMA – MUDA DK 75**

**KUSUDI**

Kutoa vitangulizi kiwango na hitaji la klab kuwa na muundo.

**LENGO:**

Kueleza hatua za msingi na sera za kufaa katika kuanzisha chama.

**MAELEZO**:

Watu wanapaswa wajifunze maeneo matatu makuu

1. **MUUNDO WA CHAMA**
   a) Kujitoa kwa kanisa- kila kanisa linapawa liweke nafasi muhimu ya kuunda klab ya wavumbuzi ya vijana wa kiume na wa kike katika vikundi vya vijana 4 – 8
   b) Kanisa – mkurugenzi – msaidizi, karani, mshauri, mzazi.

c) Jedwali la mtiririko wa muundo wa uopngozi wa kanisa

**Fedha – Fedha za chama zinapatikanaje?**

a) Ada ya wanachama – yaweza kutolewa kwa mwezi/robo au kwa mwaka inategemea na wanachama walivyokubali.
b) Michango – marafiki wadhamini wazazi na wale wote wanaopenda kuona vijana hawa wanapata malezi yafuatayo – watatoa na pia wataombwa kutoa.
c) Sadaka – Kanisa litapanga kutoa sadaka kwa ajili ya vijana hawa – mkurugenzi kwa kupitia baraza watapeleka mapendekezo kwa baraza la kanisa kukubaliwa itolewe.
d) Mahusiano ya jamii – program za klab zinapaswa zitambulike.

**2. SERA ZA KUENDESHA**

a) Baraza la kanisa
b) Kuhusika kwa wazazi
c) Uanachama
   i. Kijana wa miaka 6 – 9
   ii. Kukubali kushiriki kazi zote za chama
   iii. Uwe tayari kuhudhuria kazi na mikutano
   iv. Wazazi wakubali kijana kushiriki

**Sare**

Sare inafanya muundo uwe hakika. Ndiyo inayoleta uenyeji na umaana wa muundo, inaweka kiwango bora cha mwanachama unapokosa sare kiwango kinadhihirisha kipo chini. Sare zinafanya program kupendeza.

**Kalenda:**

a) Kalenda ya vijana hawa ni ya miezi 9
b) Program za wavumbuzi zinapaswa ziwe 4 kwa mwezi
c) Panga shughuli za uinjilisti
d) Kambi la familia
e) Matembezi


Usafiri 1 uwe kijana wa miaka

**Fomu ya afya**

Mtoto anapaswa ajaze fomu inayoonyesha afya yake, kama kuna tatizo kiafya lielezwe linavyotibiwa.

Hatua za kuunza na kuunda.

**JEDWALI LA MTIRIRIKO WA MUUNDO WA KANISA**




**SEHEMU YA TANO KIPINDI DK 120**

**KUPANGA PROGRAM ZA CHAMA**

**Makusudi:**
Kuwasaidia watoto kujenga urafiki na Yesu kuwaongoza kuelekea uzima wa milele na kuwaimarishia mahusiano yao na wazazi.

**Lengo**:
Kuelewa na kutekeleza program za wavumbuzi yaliyomo yafuatwe na kuonyeshwa na vile mtu ashiriki.

**Maelezo:**
1. **Malengo-** Unapopanga program unapaswa kujiuliza maswali yafuatayo

i. Unataka kukamilisha nini?
ii. Utakamilisha kivipi?
iii. Utakamilisha wakati gani?
iv. Nani atafanya
v. Je kipimo kinatambulika
vi. Hatua za mawasiliano

2. **PROGRAM ZA MWAKA**

**a) Yafuatayo yanapaswa kufikiriwa na kiongozi**

i. Unataka kukamilisha nini kwa mwaka huu lengo lako ni nini?
ii. Wavumbuzi wanataka kufanya nini?
iii. Matatizo ya wavumbuzi yanafahamika umeyapanga. Mfano siku ya wavumbuzi, Biblia wakati wa likizo, makambi nk.
iv. Vifaa vya madara na maburudisho
v. Mitaala ya wavumbuzi ipo?
vi. Kuwepo kila mwaka mada kuu ya chama kule unakolenga.
vii. Anza na kumaliza kwa wakati program zako
viii. Kila program ipangwe kutegemeana na mazingira.
ix. Panga pia semina ya wazazi
x. Wasilianana Conference yako kujua mambo muhimu ya mwaka.

**b) PANGA KALENDA**

Kalenda ipangwe ya matukio yote. Epuka mambo ya kushitukiza. Kalenda ya wavumbuzi tunachukulia kuwa inapaswa ichukulie miezi 9 kukamilisha matakwa yaliyoko kwenye kadi lakini waweza kuwa na zaidi ya hapo.

Kalenda ihusishe:-

i. Mafundisho ya mtaala wa darasa wenye mahitaji yaliyoko kwenye kadi.
ii. Shughuli za robo, mwezi, wiki
iii. Mikutano – kila mkutano watumie

**KUJIHUSISHA KWA WAZAZI**

Wazazi wanapaswa kutambuliwa kuwa ndiyo ufunguo mkuu wa mahusiano ya huduma hii, waonwe kama wainjilisti wa kwanza kwa motto, mvuto wao ni muhimu sana kwa mafanikio ya huduma ya wavumbuzi, kiongozi anapaswa kuelewa ulimwengu wa wazazi wa wavumbuzi, ili ufanikiwe katika huduma. Saidia wazazi kutimiza mahitaji ya watoto. Pia kiongozi unapaswa kuelewa aina ya wazazi.

Yako makundi 6 angalia mwongozo uk.

3. **MIKUTANO YA CHAMA**

**a) Uanachama**

i. Ni vijana wa miaka 6 – 9/ darasa la 1 – 4 anaruhusiwa.
ii. Atoe ada ya uanachama
iii. Mzazi atoe ukubali wake kwa huduma
iv. Awe tayari kufanya shughuli zote za chama

b) Wasiyowanachama

4. **SHUGHULI ZA WAZAZI NA WATOTO**

Lengo kuu hapa ni kukomaza uhusiano wa mzazi na motto kwa kuwafanya washirikishe vitu Fulani vya maana katika maisha katika ulimwengu wa wengine.

Mfano:

Watoto: - Masimulizi ya visa vya Biblia
- Kucheza
- Kugundua vitu vilivyofichwa
- Kucheza na mwanasesele

Wazazi - Duka la kuuza vitu
- Kufanya kazi shambani/bustani
- Kusafisha vyombo
- Kutayarisha chakula
- Kuosha baiskel, gari nk.

Kazi zinaweza kubadilika kila mwezi.

5. **MIPANGO**

Eleza maana ya program za wavumbuzi
Eleza yote yanayohusu chama
**Usafiri** – Ni muhimu ili wanaposafiri waelewe
Mipango ya mtandao wa wazazi
Kufanyike utaratibu wa washiriki kufahamu
Kunahitaji washiriki wajue mambo yanayoendelea katika chama
Tangaza shughuli zote
Fanya watu wafahamu shule zote za wavumbuzi
**HIKING** – Watembee matembezo maalumu
**FIELD TRIP** – Kuwepo siku ya kuvisha.

Huduma ya kuwaingiza katika shughuli za chama.
Huu ni wakati wa mkutano wa wavumbuzi ambapo wanachama na wazazi wanahitajika kumfanyia Mungu kazi.

**AHADI YA BIBLIA**

Naahidi kuwa mtii kwa Biblia Neno takatifu la Mungu na nitalichukua kama taa ya miguu na mwanga wa Njia yangu, na kufanya mara na maneno yaliyomo na kuyaweka katika moyo wangu ili nisije nikamtenda Mungu wangu dhambi.

**SIKU YA KUVISHWA**

## SEHEMU YA SITA

## NAMNA YA KUFUNDISHA MTAALA WA WAVUMBUZI

**KUSUDI:**
Kuelewa mtaala wa wavumbuzi kuona mawazo yanayohitaji mtazamo maalumu kwa anayeshiriki.

**LENGO:**
Kutoa ushauri namna ya kufundisha mtaala wa wavumbuzi katika hali ya ubunifu na yenye kuleta maana kwa watoto.

**MAELEZO**:

1. Malengo ya wavumbuzi
   Mtaala wa wavumbuzi umekusudia
   i. Kufanya watoto watoe maisha yao kwa Yesu
   ii. Wapate mtazamo chanya, katika kuishi maisha ya ukristo.
   iii. Wapate tabia, ujuzi na maarifa yanayohitaji kuishi kwa ajili ya Yesu leo.

2. Mtazamo wa ujumla
   Mtaala wa wavumbuzi unakusudia kuwatazamisha vijana katika mambo tofauti ya watoto wa ulimwengu wanamoishi na kila lengo limegawanywa katika mambo ya msingi 3
   i. Utayari
   ii. Wajibu
   iii. Kutia moyo.

   **Mambo hayo matano ni**
   i. Mahitaji ya msingi
   ii. Mungu wangu
   iii. Mimi mwenyewe
   iv. Familia yangu
   v. Dunia yang u

3. Namna ya kutumia vifaa vya mitaala
   Hakikisha unafahamu unavyofaa kwa kila hitaji la mtaala

4. Kupanga kwa ajili ya mafanikio
   i. Elewa ubunifu
   ii. Soma vyama mtaala wako kile unachokwenda kujifunza, ukielewa wewe kwanza.
   iii. Soma maelezo ya mipango yako vizuri unavyo kwenda kufundisha.
   iv. Shughulika na changamoto maalumu.
   v. Mtaala wa shule.

5. Tengeneza kalenda yako na ifanyie kazi
   i. Tambua mahitaji muhimu yanayopendelewa
   ii. Chagua njia sahihi ya kufuatisha kwa kazi zako.
   iii. Tambua nani anakwenda kufundisha
   iv. Hitaji litafundishwa lini
   v. Litafundishwa wapi

vi. Ni habari gani wanayopaswa kuifahamu
vii. Utafundishaje.

**Vyanzo**
Uwe na vifaa vyote vinavyohitajika

<u>Mambo 9 ya kuzingatia yanayowezesha kufundisha vyama na kwa kufaulu</u>

i. Anza na mipango yako vyema
ii. Fahamu mahitaji ya watoto
iii. Tafakari uelewa wao
iv. Tafakari vitu wanavyohitaji
v. Panga vizuri kazi zako
vi. Panga muda wa darasa
vii. Kusanya vitendea kazi
viii. Fundisha mtoto siyo watoto
ix. Tathimini kazi yako.

## SEHEMU YA SABA ADV. Manual pg 158

## MTANDAO WA WAZAZI

**MAKUSUDI:**
Kufundisha mbinu za malezi ya mafanikio na kupokea mibaraka ya Mungu.

**MALENGO:**
Kuhimiza umuhimu wa uwajibikaji katika malezi madaraka na majukumu ya kufundisha watoto namna ya kutii wazazi.

**MAELEZO:**

1. **UWEZESHAJI WA MALEZI**
   Tunapaswa kutambua kuwa chama, kanisa, shule, wazazi vyombo hivi vinahitaji vifaa kazi yake karibu sana kusaidia watoto hawa kupata malezi bora na pia kuwawezesha kukamilisha mahitaji yao.
   Chama kifanye kazi yake kwa kuwa husisha wazazi na kanisa na wazazi wanapaswa kuwa karibu na chama.

2. **FAMILIA YA WAVUMBUZI**
   Chama cha wavumbuzi kipo ili kuwasaidia na kuwaunga mkono wazazi katika jukumu la kulea watoto na kuwafanya wampokee Yesu.

3. **MTANDAO WA MIKUTANO YA FAMILIA YA WAVUMBUZI**
   a) Mahusiano ya malezi
   Ulimwengu wa wavumbuzi kitovu chake ni familia, ili kuyaongoza maisha ya watoto kwa Mungu ushirikiano wa wazazi na familia unahitajiwa uratibeshwe kwa hali zote.

b) Vyanzo vya jamii

Pia ni muhimu au washiriki wanapaswa kufahamu nini watoto hawa wanachojifunza jamii/washiriki pia ni chanzo kizuri cha malazi ya vijana hawa.

c) Mtandao wa program

Kunapaswa kuwepo mtandao mzuri wa kazi ya wavumbuzi na wazazi kuhusu program zinazoendelea.

4. **MTANDAO WA FAMILIA YA WAVUMBUZI KAMA UTARATIBU WA KUUNGA MKONO**.

**a) Lengo**

Kutoa mafundisho kunafaidisha familia na kutoa vifaa vya kufundishia.

b) **Kujihusisha kwa familia**.

Wazazi wanakaribishwa na kuombwa kuchukua sehemu katika shughuli za chama, kando ya mikutano ya kawaida ya wazazi wanakaribishwa na kuithamini mikutano hiyo ushirika na vijana kutoa mvuto wao na msaada.

**c) Mtandao wa familia ya wavumbuzi**

Katika eneo hili kuna mashauri kwa wazazi kusaidia kazi ya wavumbuzi wazazi ambao – inachukuliwa kuwa ni aliyezaa, malezi baraza la kanisa, idara ya familia na kaya, shule sabato watoto, idara ya watoto zinapaswa kuunga mkono wazazi kukuza tabia ya wavumbuzi.

- Sehemu hii inatoa mawazo halisi namna ya kumsaidia kiongozi kupanga vitu vya kumtia na kufanya mikutano ya wazazi iwe ya kupendeza.

**d) Vyanzo vya jumuia**

Jumuia inapaswa iwe na mtazamo chanya kwa chama cha wavumbuzi watambue kuwa hapa ndipo mwanzo mkuu wa kujenga tabia ya watoto, walione na kuliwekea umuhimu kuliko program zote.

**Kuthibitisha kwa malezi**

Mtandao wa familia

Ni sehemu inayo mtayarisha mzazi kupata nafasi ya kumsaidia motto kufikia malengo ya chama cha wavumbuzi.